

TAARIFA KWA UMMA

KUONDOA ZUIO LA UINGIZAJI WA BIDHAA ZA NYAMA KUTOKA AFRIKA KUSINI

Mnamo tarehe 8 Machi 2018 Wakala wa chakula, Dawa na Vipodozi -**ZFDA** ilizuia rasmi uingizaji wa bidhaa za nyama kutoka Afrika Kusini kutokana na kutangazwa kwa mripuko mkubwa wa maradhi ya Listeria (**Listeriosis Outbreak**) nchini humo.

Ugonjwa huu wa Listeria unasababishwa na vimelea vya bakteria aina ya *Listeria monocytogenes* ambao hupatikana katika udongo, maji na mboga mboga. Bidhaa za chakula zitokanazo na wanyama na mboga mboga zipo katika hatari zaidi ya kubeba vimelea hivi. Wanyama na binadamu hupata maambukizi ya ugonjwa huu kutoka katika vyanzo hivi vyenye vimelea vya *Listeria*.

Kutokana kutangazwa kwa upungufu wa matukio ya ugonjwa huo na Idara ya Afya nchini humo (South Africa Departement of Health) **ZFDA** inaondoa zuio hilo kuanzia leo tarehe **31.10.2018** kwa kuweka tahadhari zifuatazo:

Waingizaji wote wa bidhaa tajwa hapo juu wataendelea kufuata taratibu zote za uingizaji wa bidhaa za Chakula ikiwemo kufanyiwa ukaguzi wa kiwanda (**GMP Inspection**) kinachozalisha bidhaa hizo kabla ya kuanza taratibu za uingizaji.

ZFDA inawashauri wananchi na jamii yote ya Zanzibar kuondokana na mazoea ya kutumia vyakula bila kuvipika ipasavyo, hali inayoweza kupelekea kupata maambukizi kupitia vimelea vilivyo hai, kuepuka kuhifadhi vyakula kwa kuchanganya vile vilivyokuwa tayari kwa kula na ambavyo havijapikwa ili kuepuka kuambukiza chakula kilichokua tayari kuliwa. Pia inasisitizwa kujenga na kuendeleza tabia ya kuosha mikono kwa maji safi na salama kabla na baada ya kula

Ahsanteni.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mtendaji

Wakala Wa chakula,Dawa na Vipodozi Zanzibar

Kwa taarifa Zaidi wasiliana na:

Wakala wa Chakula na Dawa (ZFDA) kupitia barua pepe

info@zfda.go.tz

